**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. MCC/E.40/6/VOL. III/13** **14/04/2022**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya amepata kibali cha ajira mbadala cha tarehe **15 Machi, 2022** chenye **Kumb.Na.FA. 170/364/01 "B"/29** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,Hivyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi ifuatayo:-

## 1 DEREVA DARAJA II – NAFASI (7)

### *1.1 SIFA ZA MWOMBAJI*

Waombaji wawe na cheti cha kidato cha Nne (form IV) na leseni ya daraja la E au C.1 ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka (1) bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### *1.2 MAJUKUMU*

i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
v) Kujaza na kutunza taariza za safari zote katika daftari la safari,
vi) Kufanya usafi wa gari na,
vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake wa kazi.

Ofisi Kuu ya Halmashauri ya Jiji, Mtaa wa Soko Kuu, S.L.P 149, Mbeya, Simu: +255 25 2502372, Nukushi:+255 25 2502488,Barua pepe:cd@mbeyacc.go.tz,Tovuti:www.mbeyacc.go.tz

### 1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya serikali yaani TGS B.

## 2. MASHARTI YA JUMLA

i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.

ii) Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.

iii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculam Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

iv) Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma na cheti cha kuzaliwa.Muombaji atakayewasilisha"Result slip" "Statement of results" "Provisional results" au "Transcript".**HAVITAKUBALIKA.**

v) Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).

vi) Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

vii) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili.

viii) Waombaji waandike namba ya kitambulisho cha Taifa katika barua za maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

ix) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 28/04/2022 saa 9:30 Alasiri.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,**
**Halmashauri ya Jiji la Mbeya,**
**S.L.P 149,**
**MBEYA.**

**Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.mbeyacc.go.tz .**

Tangazo hili limetolewa na:-

Triphonia A. Kisiga

MKURUGENZI WA JIJI HALMASHAURI YA JIJI MBEYA

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.**